**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI**

## TAARIFA KWA UMMA

### UFAFANUZI WA TAARIFA INAYOSAMBAA MITANDAONI KUHUSU BAADHI YA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI WILAYANI MISSENYI KUWAAGIZA WANAFUNZI VYUMA CHAKAVU

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi inapenda kuutaarifu Umma kuwa inafuatilia taarifa inayosambaa mitandaoni ikidai kuwa baadhi ya Walimu wa Shule za Msingi zilizopo Tarafa ya Kiziba Wilayani Missenyi, wamekuwa na utaratibu wa kuagiza wanafuzi vyuma chakavu ambavyo vimekuwa vikiuzwa kwa ajili ya manufaa yao binafsi ya kujipatia kipato. Vilevile, taarifa hiyo imeeleza kuwa, baadhi ya wanafunzi wanaofeli masomo au kufanya kosa hupewa adhabu ya kuagizwa vyuma chakavu.

Kutokana na taarifa hiyo, Uongozi unapenda kuutarifu umma kuwa umeanza ufuatiliaji ili kubaini kama taarifa hiyo ina ukweli wowote ama la! na endapo itabainika kuwa kinachozungumzwa kwenye taarifa hiyo kina ukweli hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya Walimu hao.

Aidha, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi inawatoa shaka wananchi wote ambao kwa namna moja ama nyingine taarifa hii imezua taharuki kwao, kuwa wasiwe na wasiwasi kwakuwa Uongozi unafuatilia kwa karibu juu ya vitendo vilivyotolewa taarifa.

Imetolewa na;

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmasahuri ya Wilaya ya Missenyi
03 Juni, 2025

S.L.P 38 Kyaka, Simu: +255 28 298 2836, Nukushi: +255 28 298 2834, Barua pepe: ded@missenyidc.go.tz, Tovuti: www.missenyidc.go.tz